Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2514 JUMATANO JANUARI 29, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# BENKI YA AfDB YASIFU UONGOZI WA DKT SAMIA

>> **Juhudi** zake kuleta maendeleo zawakuna viongozi wa Afrika

>> **Mkutano** kupaisha utalii wa Tanzania Afrika na duniani Uk.2




*Sehemu ya Wakuu wa nchi 20 za Afrika wakionyesha Azimio la Dar es Salaam la kuwafikishia Umeme Waafrika Milioni 300 ifikapo mwaka 2030 katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Afrika kuhusu Nishati uliofanyika kwa siku mbili kuanzia Januari 27 hadi 28, 2025 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.*

## Dkt. Samia ataka asilimia 80% Nishati safi ya kupikia

Uk.4

## Lissu atamani mapokezi Kama ya viongozi wa CCM



Ilidaiwa kuwa Lisu alitakiwa kuripoti ofisini siku tatu baada ya uchaguzi ule, lakini bahati mbaya mbele yao kukawa na matukio makubwa ya CCM ukiwemo mkutano Mkuu uliofanyika Dodoma na kisha mapokezi ya Wassira Jijini Dar na Dk Mwinyi Zanzibar.

Uk.2

## Ushindi wa CCM unatokana na utekelezaji wa ilani yake ..Uk.5

# BENKI YA AFDB YASIFU UONGOZI WA DKT SAMIA

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Akinwumi Adesina, akiwa ni mmoja wa wajumbe waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Nishati uliofanyika kwa siku mbili mfululizo katika ukumbi wa mikutanoi wa Kimataifa Mwalimu Julius Nyerere Jijini Dar es salaam, alishindwa kuficha hisia zake na kumtamka wazi kwamba Tanzania ni nchi inaypiga hatua za haraka za kimaendeleo na akausifu uongoizi wa rais wa Awamu ya Sita Dkr samia Suluhu Hassan.

Alimtaja kiongozi huyo kuwa ni mfano wa kiongozi anayeonekana akifanya kila juhudi kuhakikishga taifa analoliongoza linapiga hatua za haraka, ikiwemo miakati yake ya kusambaza umeme Vijijini ili kuwaondoa Watanzania katika unyonge na umasikini.

Katika mkutano huo uliohudhuriwa na Marais wa nchi 25, Mawaziri wa Kisekta pamoja washirika wa maendeleo kutoka duniani kote, Rais huyo (AfDB), nchi nyingi zimekuwa zikishuhudia idadi kuwa ya wananchi wake hawapati nishati hiyo na juhudi zake zimekuwa za taratibu sana lakini Tanzania inaonekana inapiga kasi huku rais wake akisimamia kila eneo linalohitaji maendeleo.

Vilevile alimshukuru Rais Ghazouani wa Mauritania ambaye ndiye Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, kwa kushirikiana katika kufanikisha mkutano huo muhimu, akisisitiza kwamba ushirikiano huo ulitokana na dhamira yake ya kuona waafrika wanakuwa kitu kimoja hasa wanapojali masuala yanayohusu nchi zao. Mkuu huyo alisema mkutano huo ni muhimu kwa vile unajadili jambo muhimu kwa vile umeme unaopigiwa kelele kwa dunia ya sasa si anasa, bali ni maisha na ndiyo msingi wa maendeleo ya kiuchumi barani Afrika. inaendelea Uk 3

Alitoa mfano jinsi Afrika ilivyoweza kuingia hasara ikipoteza Pato lake (GDP) Afrika kwa asilimia 2 hadi 4 kwa mwaka. *Inaendelea Uk 3*




# DKT SAMIA ATAKA ASILIMIA 80% NISHATI SAFI YA KUPIKIA

NA MWANDISHI WETU

BAADA ya kufikia tamati kwa Mkutano Mkuu wa Nishati jana uliohusisha idadi kubwa ya viongozi wakuu wa nchi Marais, Mawaziri wa Kisekta, Mawazi Wakuu, makamu wa rais na wadau mbalimbali wa maendeleo, Rais wa Tanzania ataendelea kuwa kinara katika utekelezaji wa mpango wa kuifikisha tanzania katika ndoto ya kuachana na nishati chafu na kukimbilia mabadiliko ya kutumia nishati safi.

Mpango hu wa matumaini upo kayika mkakati wa kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia unaolenga kupandisha kiwango cha matumizi yake kutoka chini ya 10% hadi 80% ifikapo mwaka 2034.

Mpango Mahsusi utatusogeza karibu zaidi nia ya kufikia kufikia malengo hayo yatakayowawezesha akina mama na wasichana kuondokana na tishio la kuathirika afya zao kutokana na matumizi ya kupikia nishati chafu, kama kuni na mkaa.

Kwa mujibu wa Naibu waziri Mkuu na waziri wa Nishati Doto Biteko, amesema kuwa, Rais wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kukuza upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika, jitihada ambazo zimeungwa mkono na mkakati wa kitaifa na kujumuishwa katika Azimio litakalotiwa saini katika mkutano huu, huku akitoa wito wa ahadi na ushirikiano zaidi katika kuboresha upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani mwetu. Aidha, amesisitiza kuwa ifikapo mwisho wa mwaka 2025, uwezo wa Tanzania kuzalisha umeme utaongezeka hadi megawati 4,000, nishati inayotoka kwenye vyanzo safi na mbadala inavyonufaisha wakazi wa vijijini na mijini, huku miundombinu ya umeme ikifikia vijiji vyote 12,318 nchini.

Pia, Tanzania inaimarisha muunganiko wa Afrika kwa kuwa na miundombinu ya umeme inayounganisha nchi za Kenya, Burundi, Rwanda, na Uganda, huku miundombinu ya kuunganisha Zambia ikiwa inaendelea.

Ametaja miongoni mwa mambo mengine yatakayofanyika katika mkutano huo kuwa ni kushirikishana uzoefu; kupata ahadi muhimu za kisiasa; kutumia ushirikiano ili kufungua uwekezaji wa sekta binafsi; kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati; na kukubaliana mfumo wa ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kiashiria cha Ufuatiliaji wa Maazimio ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye Mkutano huo.

# CHADEMA WATAMANI MAPOKEZI KAMA YA VIONGOZI WA CCM

NA MWANDISHI WETU

KATIKA kuonyesha kuwa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kinatamani kujipima ubavu dhidi ya chama Tawala CCM, nao wameandaa mapokezi ya Mwenyekiti wake mpya Tundu Lissu, ambaye anatarajia kupokewa rasmi katika ofisi zao zilizopo Mikocheni Jijini Dar es Salaam.

Imeelezwa kuwa kuchelewa kwa kupokewa kwa kiongozi waao huyo aliyechaguliwa tangu Januari 21, 2025, akimbwaga mtangulizi wake Freeman Mbowe kulitokana na kupisha shamra shamra za mapokezi ya viongozi wa CCM, akiwemo Makamu mwenyekiti Bara Mzee Steven Wassira na Dkt Hussein Mwinyi aliyepokewa mjini Zanzibar.

Awali ilidaiwa kuwa Lisu alitakiwa kuripoti ofisini siku tatu baada ya uchaguzi ule, lakini bahati mbaya mbele yao kukawa na matukio makubwa ya CCM ukiwemo mkutano Mkuu uliofanyika Dodoma na kisha mapokezi ya Wassira Jijini Dar na Dk Mwinyi Zanzibar.

Kuona hivyo Chadema wakaahirisha sherehe zao zote ili kupisha zile za CCM na leo ndiyo siku waliyoona inafaa kufanya tukio lao hilo, ambapo pia imezingatia kumalizika kwa Mkutano Mkuu wa Nishati uliofanyika juzi na jana Jijini Dar es Salaam na kushirikisha viongozi wakuu wa Afrika.



# BENKI YA AFDB YASIFU UONGOZI WA DKT SAMIA

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Akinwumi Adesina, akiwa ni mmoja wa wajumbe waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Nishati uliofanyika kwa siku mbili mfululizo katika ukumbi wa mikutanoi wa Kimataifa Mwalimu Julius Nyerere Jijini Dar es salaam, alishindwa kuficha hisia zake na kumtamka wazi kwamba Tanzania ni nchi inaypiga hatua za haraka za kimaendeleo na akausifu uongoizi wa rais wa Awamu ya Sita Dkr samia Suluhu Hassan. Alimtaja kiongozi huyo kuwa ni mfano wa kiongozi anayeonekana akifanya kila juhudi kuhakikishga taifa analoliongoza linapiga hatua za haraka, ikiwemo miakati yake ya kusambaza umeme Vijijini ili kuwaondoa Watanzania katika unyonge na umasikini.

Katika mkutano huo ulihudhuriwa na Marais wa nchi 25, Mawaziri wa Kisekta pamoja washirika wa maendeleo kutoka duniani kote, Rais huyo (AfDB), nchi nyingi zimekuwa zikishuhudia idadi kuwa ya wananchi wake hawapati nishati hiyo na juhudi zake zimekuwa za taratibu sana lakini Tanzania inaonekana inapiga kasi huku rais wake akisimamia kila eneo linalohitaji maendeleo.

Vilevile alimshukuru Rais Ghazouani wa Mauritania ambaye ndiye Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, kwa kushirikiana katika kufanikisha mkutano huo muhimu, akisisitiza kwamba ushirikiano huo ulitokana na dhamira yake ya kuona waafrika wanakuwa kitu kimoja hasa wanapojali masuala yanayohusu nchi zao.

Mkuu huyo alisema mkutano huo ni muhimu kwa vile unajadili jambo muhimu kwa vile umeme unaopigiwa kelele kwa dunia ya sasa si anasa, bali ni maisha na ndiyo msingi wa maendeleo ya kiuchumi barani Afrika.

Alitoa mfano jinsi Afrika ilivyoweza kuingia hasara ikipoteza Pato lake (GDP) Afrika kwa asilimia 2 hadi 4 kwa mwaka.

Pamoja na hayo Rais huyo alieleza kutokata tamaa kwani ana matumaini makubwa tangu walipoasisi Mpango wa Nishati Mpya kwa Afrika, uliobuniwa na AfDB mwaka 2016, ambao ulileta tija na matarajio mapya.

Mpango huo uliweza kuongeza asilimia ya upatikanaji wa umeme barani Afrika na kuongezeka kutoka asilimia 39 mwaka 2015 hadi asilimia 52 mwaka 2024, na watu milioni 25 walinufaika moja kwa moja.

Dkt. Adesina alieleza kwamba watu milioni 571 barani Afrika bado hawana umeme, wakiwa sehemu kubwa ya asilimia 83 ya watu wasio na umeme duniani. hiyo ni zaidi ya watu bilioni 1 wasiokuwa na suluhisho la nishati safi ya kupikia, jambo ambalo linaathiri vibaya afya ya wanawake na watoto.

Hali hii ilipelekea kuzinduliwa kwa mpango kabambe wa Mission 300, unaolenga kuwapatia umeme watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030. Mpango huu, uliozinduliwa kwa kushirikiana na Rais wa Benki ya Dunia, Ajay Banga, umeungwa mkono na wadau wakubwa wa maendeleo kama Tume ya Umoja wa Afrika na Rockefeller Foundation.

Katika hali ya kuonesha mshikamano wa kimataifa, washirika mbalimbali wa maendeleo walitangaza ahadi zao za msaada kwa Mission 300. Dkt. Adesina aliainisha baadhi ya msaada huo, ikiwa ni pamoja na: Dola bilioni 2.5 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kiislamu, Dola bilioni 1.5 kutoka Benki ya Miundombinu ya Asia, Dola bilioni 2 kutoka Mfuko wa OPEC. Aidha, alisema serikali ya Ufaransa inatarajiwa kutoa tangazo kubwa la msaada.

Mpango mwingine muhimu ulioelezwa na Dkt. Adesina ni 'Desert to Power', ambao utaendeleza megawati 10,000 za nishati ya jua katika nchi 11 za ukanda wa Sahel na kuwapatia umeme watu milioni 250. Alisisitiza kuwa kwa kushirikiana, Mission 300 na Desert to Power zitawawezesha Waafrika milioni 550 kupata umeme ifikapo mwaka 2030.

Alisisitiza umuhimu wa kushirikiana viongozi wote wa Afrika kufanikisha malengo haya, akisema, juhudi hizi zitaacha rekodi katika mataifa ya Afrika, hata viongozi watakaokuja hapo baadaye hawataanza tena kuangalia hapa wanaposhikilia viongozi wa Afrika ya leo.



# Tanzania yafunga historia mkutano wa nishati Afrika

NA MWANDISHI WETU

HATIMAYE Mkutano Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati, uliofanyika Januari 27 na 28, 2025, umefikia tamati jana jioni huku wageni mbalimbali wakiwemo Marais, Mawaziri wa Kisekta pamoja na wadau wa maendeleo wakieleza kuridhishwa na maandalizi pamoja na mada zilizotolewa na viongozi mbalimbali.

Mkutano huo ulifungwa na mwenyeji Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni rekodi ya kipekee kwake katika Utawala wa Awamu ya Sita kushuhudia wenyeji wa mkutani mkubwa kiasi hicho uliohusisha zaidi ya nchi 25.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Wakuu wa Nchi 25, Makamu wa Rais wawili, Mawaziri Wakuu wanne, na Naibu Mawaziri Wakuu wawili, na kufanikisha idadi ya viongozi wa ngazi za juu 35" kwa Tanzania haijawahi kupokea idadi kubwa ya viongozi wa ngazi ya juu kama hawa katika tukio moja.

Katika historia Tanzania iliwahi kupokea Wakuu wa Nchi ilifikia idadi ya 19 wakati wa kifo cha Baba wa Taifa, Hayati Julius Kambarage Nyerere mwaka 1999, na Wakuu wa Nchi 15 wakati wa Mkutano wa SADC mwaka 2019.



Mkutano huu unazidi kwa ukubwa," alisema Balozi Kombo.

Nchi zilizoshiriki kwa namna moja au nyingine ni pamoja na Algeria, Kenya, Nigeria, Ghana, Ethiopia, Zambia, Sudan, Kenya, Nigeria, Libya, Somalia, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na nyinginezo. Makamu wa Rais kutoka Gambia na Benin pamoja na Mawaziri Wakuu kutoka Cote d'Ivoire, Uganda, São Tomé and Príncipe na Equatorial Guinea watashiriki pia.

Balozi Kombo alibainisha kuwa mkutano huu ni matokeo ya juhudi za diplomasia ya kimataifa zinazotekelezwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Mwaliko wa Rais Samia katika Mkutano wa Nchi 20 Tajiri zaidi duniani (G20) nchini Brazil Novemba 2024, na nafasi aliyopewa kuzungumza kwa niaba ya Afrika kwenye Mkutano wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya Afrika na China (FOCAC), ni ishara ya kuimarika kwa nafasi ya Tanzania duniani," alisema.

Balozi Kombo pia alisisitiza kuwa mikutano ya kimataifa kama huu ina faida kubwa kwa uchumi wa ndani, hususan sekta ya utalii, hoteli, usafiri, na wajasiriamali wadogo kama mama lishe na boda boda, akisema kuwa inatoa fursa ya kipekee ya kukuza mapato ya wananchi wa kawaida.



# Tanzania mfano usambazaji umeme Vijijini

NA MWANDISHI WETU



RAIS wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan jana aliongoza Wakuu wa nchi za Afrika katika majadiliano ya pamoja kwenye Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ‘Mission 300’.

Mijadala hiyo iliendelea kwa siku mbili za mkutano huo wa nishati unaofanyika Jijini Dar es Salaam nchini Tanzania.

Siku ya juzi mijadala ilihusisha mawaziri wa mataifa mbalimbali, viongozi wa sekta binafsi, wadau wa masuala ya maendeleo ya nishati na fedha na jana wakuu wa nchi walikuwa ni sehemu ya mkutano huo.

Baadhi ya Marais waliowasili ni pamoja na Rais wa Kenya, Sierra Leone, Malawi, Somalia, Zambia, Ethiopia, Djibout, Madagascar, Libya, Mauritania, Gambia, Burundi, Congo, Comoros, Ghana na Botswana.

Wakati viongozi hao wakiendelea kuwasili katika jiji la Dar es Salaam, hali ya usalama imeendelea kuimarishwa katika maeneo mbalimbali ya jiji.

Kwa siku hizo mbili shughuli mbalimbali zilisitishwa ikiwemo elimu mashuleni na huduma nyingine za kiserikali huku watumishi wa umma wakitakiwa kufanya kazi wakiwa majumbani.

Katika mjadala uliosisimua juzi ni Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt Akinumwi Adesina ambaye alisema, Lengo la kuwafikishia umeme watu milioni 300 Afrika linakwenda kufanikiwa, “Tunahitaji uwazi na uwajibikaji katika kufikisha lengo hili.”

Pia Adesina alisema kuwa Tanzania imekua mfano wa kuigwa kwa kufanya vizuri katika uwekezaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwafikishia nishati ya umeme wananchi katika vijijini vyote 12,318.

Miungoni mwa nchi zinazotajwa kuwa na changamoto zaidi ya nishati hiyo ni Chad, Guinea, Niger, Mali, na nchi nyingine nyingi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo zimekuwa zikikabiliwa na uhaba wa nishati kwa muda mrefu kidogo.

Kulingana na ripoti ya Wakala wa Kimataifa wa Nishati (IEA) iliyochapishwa Juni 2023, watu milioni 567, Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara hawakupata umeme mwaka 2021, ikiwa ni zaidi ya asilimia 80 ya watu wote duniani ambao hawakupata umeme.

Chad ambayo ina sera ya maji na umeme bila malipo kwa matumizi yasiyozidi kiwango cha kila mwezi cha kWh 300 kwa umeme na mita za ujazo 15 za maji, haijaeleza haswa juu ya sababu za shida ya umeme.

Lakini kulingana na Taasisi ya Thinking Africa, mzozo wa nishati nchini Chad ni matokeo ya usimamizi mbovu wa kiufundi na kibiashara, na kusababisha tatizo kubwa la umeme.

Ingawa nchi hiyo ina uwezo mkubwa wa nishati kama vile jua, majani, upepo, Jotoardhi na hidrokaboni, vyanzo ambavyo vinaweza kuchangia maendeleo ya sekta hiyo, lakini bado hawajajitosheleza.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# DKT SAMIA AAHIDI NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUFIKA 80%




NA MWANDISHI WETU

TANZANIA ni moja kati ya nchi 12 zitakazozindua Mpango Mahsusi wa Kitaifa kuhusu Nishati (National Energy Compact). Kupitia Mpango wetu tunatarajia kuongeza kasi ya kuunganisha umeme nchini, hadi kufikia asilimia 75 ifikapo mwaka 2030. Ili kufanikisha azma hiyo ndani ya muda wa miaka mitano ijayo tutahitaji uwekezaji wenye thamani ya dola za Marekani bilioni 13, ambapo dola bilioni 5 zitapatikana kutoka sekta binafsi hapa nchini. Kupitia Mpango huu tumepanga kutekeleza mambo makubwa manne.

La kwanza ni kuongeza uzalishaji wa umeme, kutokana na nishati mchanganyiko, yaani energy mix. Hadi sasa Tanzania ina uwezo wa kuzalisha MW 3,431.20, ambapo 58% ya hizo inatokana na vyanzo vya maji, 35% inatokana na gesi asilia na 7% inatokana na vyanzo vingine. Shabaha yetu ni kuongeza MW 2,463 za nishati kutokana na nishati ya jua, gesi asilia, upepo na jotoardhi na vyanzo vingine, ifikapo 2030.

Jambo la pili, Kijiografia Tanzania ni kiungo muhimu katika kuunganisha Mtandao wa Umeme kwa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika, Eastern Africa Power Pool na Southern African Power Pool, na hivyo kuwezesha biashara ya umeme kutoka Afrika Kusini hadi Misri. Tayari tumekwishaunganisha miundombinu ya umeme na nchi za Burundi, Kenya na Rwanda. Kwa sasa tunaendelea kuunganisha miundombinu ya umeme na Zambia na Uganda.

Kuwepo kwa miundombinu hiyo, itawezesha biashara ya nishati kati ya nchi za EAC na SADC, Tanzania inayo nafasi ya kuuza umeme ikizingatiwa kuwa hadi Mwezi Novemba, 2024 mahitaji ya umeme nchini Tanzania yalikuwa MW 1,888.72 wakati uzalishaji wetu ni MW 3,431.20.

Jambo la tatu ni kufikisha umeme kwenye vitongoji. Baada ya kufanikiwa kusambaza umeme katika vijiji vyote 12,318 vya Tanzania, mwelekeo wetu ni kuvifikia vitongoji vyote 64,359. Hadi sasa, tumeshavifikia vitongoji 32,827, na kazi inaendelea katika vitongoji 20,000. Hivyo, kupitia Mpango huu tutaweza kukamilisha vitongoji 11,532 vilivyobakia.

Jambo la nne ambalo Mpango huu utafanya ni kusaidia usambazaji wa nishati safi ya kupikia. Inakadiriwa watu milioni 950 barani Afrika wanakosa nishati safi ya kupikia. Hali hii inaligharimu sana bara letu, na inahusishwa na kuongezeka kwa umaskini, vitishio vya kiafya, uharibifu wa mazingira, kuongezeka kwa uzalishaji wa kaboni, kupotea kwa bioanuwai, na kukosekana kwa usawa wa kijinsia.

Nchini Tanzania utegemezi wa kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia ni zaidi ya 90%. Hatuwezi kupuuza madhara na gharama kubwa ya kutumia kuni na mkaa, hasa kwa afya na ustawi wa wanawake na wasichana.

Katika kukabiliana na hili, Tanzania tumeweka Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia unaolenga kupandisha kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia kutoka chini ya 10% hadi 80% ifikapo mwaka 2034. Mpango Mahsusi tunaouzindua leo utatusogeza karibu zaidi kufikia lengo hilo.

# TAHARIRI

## Karibuni tena Tanzania

HATIMAYE Mkutano ulioshirikisha Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati, umefikia tamati jana jioni huku wageni mbalimbali wakiwemo Marais, Mawaziri wa Kisekta pamoja na wadau wa Maendeleo kurejea katika nchi zao.

Tunaipongeza Serikali ya Tanzania hususan Rais Dkt Samia kwa heshima aliyopewa ambayo imeifanya Tanzania kuwa nchi ya mfano Afrika, iliyoandaa tukio kubwa na la kihistoria. Sisi Jamzi la Habari tumeshuhudia wajumbe wakieleza wazi kuridhishwa na maandalizi pamoja na mada zilizotolewa na viongozi mbalimbali, hatuna shaka yote haya yamefanikiwa chini ya uratibu wa serikali ya Tanzania inayopiga hatua kila uchao katika kukuza masuala ya Diplomasia.

Tunajua kwamba ugeni huu umeandika historia ya kipekee ambayo pengine haijawahi kufanyika, hivyo kwetu sisi tunawaombea wageni wetu warudi salama lakini wakifika huko tunaamini mioyo yao itabaki katika taifa hili.

Kama nchi yetu ilivyo kinara katika kutangaza Utalii, tunaamini ugeni ule utatuletea idadi kubwa ya watalii, maana tumeshuhudia baadhi yao wakieleza wazi kuvutiwa na vivutio vilivyotapakaa katika nchi hii.

Tunarudia kumtia moyo Rais pamoja na wasaidizi wake waendelee kuitangaza nchi yetu kimataifa ili tuweze kushuhudia matukio makubwa kama haya, ambayo pia yana thamani kubwa kwa ustawi wa nchi yetu

Tunajua kuwa Mkutano huo uliohudhuriwa na Wakuu wa Nchi 25, Makamu wa Rais, Mawaziri Wakuu, na Naibu Mawaziri Wakuu, na kufanikisha idadi ya viongozi wa ngazi za juu 35" kwa Tanzania haijawahi kupokea idadi kubwa ya viongozi wa ngazi ya juu kama hawa katika tukio moja.

Tunashindwa kuzipongeza nchi moja moja zilizoshiriki lakini kwa uchache tunazitaja majirani kama Algeria, Kenya, Nigeria, Ghana, Ethiopia, Zambia, Sudan, Kenya, Nigeria, Libya, Somalia, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, pamoja na viongozi waliokuwemo kama Makamu wa Rais kutoka Gambia na Benin pamoja na Mawaziri Wakuu kutoka Cote d'Ivoire, Uganda, São Tomé and Príncipe na Equatorial Guinea na wengine wote waliopata bahati ya kuhudhuria mkutano huo wa kihistoria.

Tunamuombea Rais Dkt Samia afya njema ili aendeleze dhamira yake ya kuiona nchi ya Tanzania ikipiga hatua kimaendeleo. Mungu ibariki Tanzania.

## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778,
- 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684,
- 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz




*Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria wa Wizara ya Katiba na Sheria, Ester Msambazi akizungumza kwenye mafunzo ya wataalamu wa sheria watakaotoa huduma kwa wananchi kwenye Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC) inayoanza leo mkoani Kilimanjaro.*

UCHAMBUZI

# Uahindi wa CCM unatokana na utekelezaji wa ilani yake

NA MWANDISHI WETU

SIRI kubwa ya maandalizi ya CCM Kushinda uchaguzi Mkuu na kuendelea kushika Doila, ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ambayo viongozi, waliopewa nafasi waliibeba na kuifanyia kazi kila eneo.

Hilo ndilo linaloweza kuwafanya wagombea wa chama hicho akiwemo mgombea nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la wviongozi wengine watakaopambania nafasi za Ubunge na Madiwani.

Tayari chama hicho kimefanya chaguzi za ndani kama vile ule uliohusisha Mkutano Mkuu wa CCM, ulimchagua Mzee Steven wassira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara.

Wassura aliyekuwa nje ya madaraka ya kisiasa kwa muda mrefu kwa maneno yake mwenyewe alieleza kushangazwa na ushindi ule na akaahidi kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa, kama hatua ya kulipa fadhjila na heshima ile kubwa.

Pia mkongwe huyo akatabiri ushindi wa kishindo utakaokipata chama chake, mtaji mkubwa ukiwa ni utekelezaji wa Ilani na jinsi chama hicho kinavyoendesha siasa zake kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

Mkongwe huyo ameingia na Falsafa ya Umoja Maridhiano na Ushindi, kazi ambayo amewaahidi wajumbe waliomuamini kushika wadhifa huo kuwa ataifanya kwa bidii kubwa huku akiamini ni jukumu lenye baraka za Mungu.

Kwa tathmini nyepesi ya ushindi huu wa Wasira una maana kubwa kwa CCM kuekelea uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka huu, mwezi Okttoba kwamba mtaji wake unaonekana umeongezeka

Ukichukulia kuwa CCM ndicho chama kinachoongoza nchini kwa kuwa na wanachama na wapenzi wengi kinaweza kutumia mtaji huo kumpa ushindi wa kishindo mgombea wake wa Urais na hata Wabunge na Madiwani.

CCM ina watu wengi hata isipohitaji kura ya wapinzani au watu wasiofungamana na siasa ya chama chochote bado wana uhakika wa kushinda hususa nafasi ya Urais pengine baadhi ya wabunge wachache wanaweza kupoteza viti kutokana na kutowafanyia vizuri wapiga kura wao katika kipindi kilichopita.

Mgombea wa CCM anasaidiwa na maendeleo yanayoonekana kila kona, atahitaji timu ya kawaida tu kumnadi na kuweza kumpa ushindi wa kimbunga kama huu alioanza kuonyesha dalili Mzee Wasira

Ushindi wa CCM mwaka huu unaonekana bila kuhitaji utafiti mkubwa, kwani hata ukiangalia upande wa upinzani bado unaonekana kama hakuna chama chenye nguvu kama ilivyokuwa katika chaguzi za awamu zilizoipita tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992

Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Ni mwaka tutakaoendelea kusikia vishindo vya CCM katika majimbo na makelele ya wapinzani watakaoendeleza msamiati wa kuibiwa kura ili hali hawakuwa na maandalizi zaidi ya malumbano na kukashifiana.

# Tanzania yavunja rekodi u

NA MWANDISHI WETU




JANUARI 27, 2025, Mkutano wa Nishati unaowakutanisha Marais, Mawaziri wa Nishati, Mawaziri wa Fedha, na wadau wa maendeleo uliandele kufanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere Jijini la Dar es Salaam, Tanzania.

Mkutano huu, unaojulikana kama "Mission 300", unalenga kujadili mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa watu milioni 300 Barani Afrika.

Jana Jumanne Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, alipokea Marais wa mataifa mbalimbali waliohudhuria mkutano huo.

Wakati mkutano huo ukiendelea Tanzania imeanza kupiga hatua kubwa ikijiwekea malenhgo ya kufikia sehemu kubwa ya nchi kupata nishati ya umeme, hivi karibuni Serikali iliweka wazi kuwa imefanikiwa kufikisha umeme katika vijiji 12,278, sawa na asilimia 99.7 ya vijiji vyote nchini katika kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka jana 2024.

Pia katika kipindi hichi vitongoji 32,827 vimefikiwa na umeme kati ya vitongoji 64,359, sawa na asilimia 51.

Imesema, hatua hiyo imeongeza fursa kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kuboresha sekta muhimu kama elimu, afya, biashara, na usafiri.

Hayo yamesemwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, leo Januari 5, 2025, katika ukumbi wa Maktaba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akifungua semina ya wahariri na Waandishi wa habari kujirisha Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati utakaonyika Januari 27-28, 2025, katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Msigwa amesema kwa mujibu wa takwimu, zaidi ya taasisi 12,905 za afya na elimu zimeunganishwa na umeme, hatua ambayo imeimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Amesema zaidi ya hayo Serikali imewekeza katika vyanzo mbadala vya nishati kama umeme jua, jotoardhi, na upepo, ambapo uzalishaji unatarajiwa kuongezeka kwa megawati 1,100.

"Hii inalenga kuvutia uwekezaji zaidi katika sekta ya viwanda, ambapo idadi ya viwanda vya uzalishaji wa vifaa vya nishati kama nguzo na nyaya imeongezeka kutoka 23 mwaka 2020 hadi kufikia viwanda 78 mwaka 2024.

Uzalishaji wa ndani wa vifaa hivi siyo tu unatoa ajira kwa Watanzania, bali pia unapunguza gharama za usambazaji wa nishati vijijini na mijini", alisema Msigwa.

Kuhusu Mkutano huo wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati Msigwa amesema ni matokeo ya juhudi kubwa za kidiplomasia za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

"Rais Dk. Samia ameonyesha uongozi wa mfano barani Afrika kwa kusimamia ajenda ya nishati safi ya kupikia, ambapo kupitia Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Nishati Safi wa mwaka 2024-2034, Tanzania imelenga kufikia asilimia 80 ya kaya kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Hatua hii inalenga kuboresha afya za wananchi na kulinda mazingira dhidi ya uharibifu wa misitu unaotokana na matumizi ya kuni na mkaa", alisema Msigwa.

Msigwa alisisitiza, mkutano huo utaweka msingi wa kupatikana kwa umeme kwa Waafrika milioni 300, ambapo nchi 14 za Afrika
tatia saini makubaliano ha
mbele ya marais zaidi ya
wa Afrika.

Aidha, Msigwa amew
himiza waandishi wa hab
kushirikiana kwa dhati
Serikali kufanikisha mk
tano huo, huku akibainis
kwamba Tanzania inayo
fasi ya kipekee kuimaris
taswira yake kimataifa kup
tia tukio hili.

"Ndugu wahariri
waandishi wa habari, nir
ni daraja muhimu kati

# usambazaji umeme vijijini



> ekezaji zaidi katika sekta ya viwanda, ambapo idadi ya viwanda vya uzalishaji wa vifaa vya nishati kama nguzo na nyaya imeongezeka kutoka 23 mwaka 2020 hadi kufikia viwanda 78 mwaka 2024.





zi-
yo
10

va-
ari
na
ku-
ha
na-
ha
pi-

na
nyi
ya

Serikali na wananchi. Hakikisheni taarifa sahihi kuhusu juhudi za Serikali zinawafikia wananchi.

Kupitia mkutano huu, tunawataka kuelewa kwa undani ajenda zake na kuelimisha umma kuhusu umuhimu wake," alisema Msigwa.

Msigwa alimalizia kwa kutoa mwito kwa Waandishi wa habari kuweka ajenda moja ya kuijenga taswira chanya ya Tanzania kimataifa, akisisitiza kwamba "Tanzania Kwanza!"

# TANZANIA YAZIDI KUVUTIWA KWA MAENDELEO




NA MWANDISHI WETU

MAENDELEO yanayofanyika ikiwemo ujenzi wa Miundombinu ya Barabara, Reli ya kisasa, Hospitali, Zahanati na maboresho katika sekta ya elimu ni miungoni mwa mambo yanayowavutia hata wananchi wanaoshi katika nchi jirani na Tanzania.

Wananchi wa Kenya wanapotembelea Tanzania mara nyingi wamekuwa wakiweka wazi juu ya kuvutiwa kwao na maendeleo wanayokutana nayo katika miji ya Tanzania, ambayo miaka ya nyuma walikuwa wakiiona katika nchi yao.

Kwa sasa kinachovutia Wakenya wengi ni uwepo wa Treni ya kisasa inayofanya safari zake katika miji ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma ambayo kwao wanafananisha na ile inayotumika katika nchi zilizoendelea hususan katika Bara la Ulaya na Marekani na nchi zilizoendelea.

> "Hii inatokana na mikakati ya Serikali Awamu ya sita kupitia Ilan ya Chama tawala CCM, ambayo imekuwa ikiratibu maendeleo na kuifanya nchi kuonekana ikipiga maendeleo ya kasi.

Baadhi ya Wakenya waliozungumza na gazeti hili, wanaweka wazi jisni gani maendeleo ya Tanzania wanavyoyaona yakilipita taifa lao, huku wakijiuliza nini kilichofanyika katika nchi hii jirani yao, ambacho kwao hakiwezei.

Ukiacha Wakenya hata mjirani wengine kutoka nchini Malawi nao wanayasifia maendeleo ya Tanzania, kwamba yanakuwa ni mfano wa kuigwa katika nchi za ukanda wa Maziwa Makuu, hasa kukua haraka kiuchumi na maendeleo mengine yanayoonekana wazi.

Wanakumbusha kwamba mnamo miaka ya 1990 Majiji ya Malawi kama vile Blantire, Lilongwe na hata Mzuzu yalikuwa ndiyo safi zaidi miungoni mwa nchi za jirani ikiwemo Tanzania.

Miji hiyo ndiyo iliyoanzisha mpango wa kusafishwa usiku kabla ya Dar es salaanm na Nairobi hayajaanza kupata huduma hiyo, lakini matokeo yake hivi sasa wameachwa mbali kimaendeleo.

Katika mika hiyo Barabara ya Tanzania inayounganisha nchi ya Malawi ilikuwa hajakamilika kwa kiwango cha Lami, hivyo wasafiri wanaotoka nchini walikuwa wakikutana na Barabara za Lami wanapoingia nchini Malawoi hususan katika miji ya mwanzoni kama Kalonga, Lumph, Ekwendeni na Mzuzu kisha kuelekea katika Mji Mkuu wa Lilongwe.

Hata hivyo miji hiyo kwa sasa inakabiliwa na uchakavu wa miundombinu huku Tanzania ikizidi kujenga barabara katika mikoa na wilaya ambazo awali zilikuwa zimejifunga kutoka eneo moja kwenda jingine.

Miradi ya kimkakati ya ujenzi ilianza kushika kasi tangu utawala wa Awamu ya Tano chini ya Rais Dkt hayati John Pombe Magufuli ambapo sasa ndiyo kasi imeongezeka katika utawala wa awamu ya Sita chini ya Dkt Samia Suluhu Hassan.

Kufuatia maendeleo hayo Tanzania inaelekea pazuri na pengine kwa miaka michache ijayo, itakuwa ndiyo nchi kimbilio kwa wananchi mbalimbali kutoka mataifa mengine kama ilivyokuwa Afrika Kusini, nchi inayopokea wageni kila uchao kutokana na kufunguka kwa fursa za kibiashara na maisha.

Hii inatokana na mikakati ya Serikali Awamu ya sita kupitia Ilan ya Chama tawala CCM, ambayo imekuwa ikiratibu maendeleo na kuifanya nchi kuonekana ikipiga maendeleo ya kasi.

Dkt Samia ambaye amekuwa akisimamia kwa makini masuala ya maendeleo, amekuwa mkali kwa wasaidizi wake akiwataka wasifanye ajizi inapobidi kusimamia kazi za kuwatumia Watanzania, ndiyo maana amekuwa mkali na asiyekuwa na subira pale anapogundua uzembe unafanyika sehemu yoyote il anafanya mabadiliko ya haraka.

# MAFANIKIO YA AFYA, MAJI, BANDARI NA ELIMU YATAJWA 'BIRTHDAY' YA DKT SAMIA



NA MWANDISHI WETU

MIKOA mbalimbali, taasisi, vikundi vya marafiki na wananchi mbalimbali juzi walishiriki kikamilifu kusherehea Siku ya kuzaliwa kwa Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, huku Mkoa wa Kagera ukiyataja mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika utawala wa Awamu ya Sita chini ya rais huyo hayapaswi kupita bila kupongezwa

Ukiacha shere za aina tofauti zilizofanyika katika Jiji la dar es salaam, lakini hata baadhi yao mikoa nayo imeripotiwa kufanya sherehe hizo za kumtakia maisha marefu na yenye afya kiongozi huyo wa nchi.

Kauli ya upendo nyingine imatokea mkoani Kagera kupitia Mkuu wake Fatma Mwassa ambaye alisema kuwa, Wakazi wa Mkoa Kagera kuwa hawana budi kumpongeza na kumuombea Sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan kutokana na shughuli nyingi za maendeleo zilizofanyika katika Mkoa huo. Akizungumza wakati wa sherehe za kumpongeza Mhe. Rais Dkt. Samia kwa kutimiza Miaka 65 ya kuzaliwa, zilizoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa CCM Mkoa wa Kagera (UWT), Hajat Fatma Mwassa amesema mengi yanaonekana yaliyofanywa na Dkt. Samia yakiwemo yanayohusu Elimu, Afya, Barabara, Maji, Bandari, huku mengine yakiwa yamekamilika na mengine yakiwa katika hatua za kukamilika na mengine yakianzishwa.

"kwa uchache mmeona Vituo vya Afya na Hospitali zimejengwa ni Kazi ya Mhe. Rais Dkt Samia, mmeona Shule nzuri na Watoto wetu wanasoma vizuri ni kazi ya Dkt Samia, Mmeona Bandari zetu za Bukoba na Kemondo kila moja zimeletwa Shilingi Bilioni 22 kazi inakamilika kufikia Mwezi Machi, Barabara Njia Nne zinajengwa ni Kazi ya Dkt. Samia, Maji, Barabara, Umeme mpaka Vitongojini ni mengine mengi ni kazi ya Mhe. Rais Samia.." amesema Hajat Mwassa.

Aidha ameongeza kuwa ni muda sasa wa Akina Mama hao wa CCM kuendelea kukiimarisha Chama Cha Mapinduzi kwa kumpambania Rais Dkt. Samia kuhakikisha anapata Ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba Mwaka huu, kwa kumtafutia Kura hadi chini ya Uvungu, na kuzilinda kura hizo, ili kumpa nafasi ya Miaka Mitano mingine akamilishe Miradi mingine ya Maendeleo.

Sherehe hizo za kumpongeza Rais Dkt Samia zimefanyika Kata Kashai Bukoba Manispaa na Kuhudhuliwa na Viongozi pamoja na Wanawake wa UWT kutoka Wilaya zote za Mkoa Kagera.

# Nishati ya umeme yaifungua Bagamoyo

NA MWANDISHI WETU

VIJIJI na vitongoji kadhaa wilayani Bagamoyo mkoa wa Pwani vili vkuwa giza kutokana na kutopata nishati ya umme, vingine tangu ulipopatikana uhuru wa nchi hii mwaka 1961, lakini sasa maeneo mengi wanatos shukurani kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwezesha kuondoa changamoto hiyo.

Mfano ni Kijiji cha Saadan kilichokuwa katikati ya Hifadhi hiyo ambacho awali iliyogubikwa na giza, umasikini uliochagizwa ukosefu wa huduma za kijamii na kulifanya eneo hilo lisifikike kwa urahisiu kutokea katika miji mikubwa inayolizunguka kama vile yalipo makao makuu ya wilaya, Bagamoyo na Jiji la Dar es salaam.

Nyuma ya miaka ya 1960 hakukuwa na mwanga katika eneo hilo, wenyeji walioshi eneo hilo walijikita katika kazi ya uvuvi wakitumia nyenzo duni, pia kulikuwa na biashara nyingine kama vile ukataji wa ukindu, zao lililotumika sana kwa ajili ya ususi wa mikeka na vikapu, kadhalika ukataji miti ya Mikoko iliyokuwa ikisafirisahwa kwa majahazi kwenda katika miji ya Zanzibar na hata nje ya nchi Mombasa na Visiwa vya Comoro.

Mwanga ulijitokeza mwaka 1962 ilipoanzishwa Bustani ya wanyama, iliyojmumuisha wanyama wachache waliofungiwa katika Ng'enge (Zoo) kubwa na ndogo, zilizoanza kuvuta macho ya watalii kuanza kutembelea kijiji hicho kilichokuwa na wakazi wachache, wengi wao wakitokea maeneo mbalimbali ya nchi na kuafauata biashara ya uvuvi.

Enzi za Ukoloni Saadani iliwahi kukaliwa na Koloni la Waarabu walioendesha biashara ya utumwa, iliyotanabaishwa na kuwewpo mabaki ya magofu machache yaliyokuwa yakitumiwa katika biashara hiyo, pia gati kuu la kusafirishia watumwa kutoka bandari ndogo ya Saadani kuelekea Unguja na nchi nyingine za jirani.

Kwa mujibu wa simulizi za wazee wa mji huo hata jina hili la Saadani, lilitokana na Mzee mmoja wa Kiarabu aliyekuwa akimiliki saa ya ukutani, hivyo alipochoshwa na maswali ya kuulizwa muda "Saa ngapi? kila mara akawa anawajibu "kama unataka saa nenda kaangalie ndani.

Kwa vile hakuweza kutamka vizuri maneno ya Kiswahili ndipo alipokuwa akikatisha tu kwa kusema "Saadani" ndipo likazaliwa jina hili.

Ukuaji wa mbuga hiyo ya wanyama iliweza kuupa umaarufu mji huo mdogo ulipo kandoni mwa Bahari ya Hindi kwa kuanza kutembelewa na watalii pamoja na watu maarufu, akiwemo Mwanasiasa aliyeshika nyadhifa mbalimbali serikalini Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyefika Saadani Mwaka 1974 na kuweka jiwe la Msingi la kumbukumbu ya ujiuo wake na uzinduzi wa bustani hiyo ya wanyama.

Kwa bahati nzuri kijiji cha saadan kiliweza kuonja maendeleo mapema kwa kupata zahanati pamoja na Shule ya Msingi iliyoanza ikiwa na madarasa manne na baadaye ikaendelea na kukamilisha madarasa yote saba, pia kiliwahi kununua gari aina ya Center kwa ajili ya shughuli za kijiji.

Kupitia uwepo wa bustani hiyi ya wanyama kijiji nhicho kilianza kupokea wafanyakazi wengi wakati huo wakijulikana kama 'Game Scout' kutoka maeneo mbali mbali na baadhi waliajiriwa wananchi wakazi wa kijiji hicho na vile vinavyozunguka bustani hiyo kama Uvinje, Buyuni Kuu na Buyuni Kitopeni.

> *Kufuatia kupatikana kwa nishati hiyo kijiji cha Saadan kilichokuwa kikikumbana na matukio ya kuvamiwa na wanyama wakati na waharibifu kama vile Tembo na Simba sasa imepungua na kuwa sehemu salama toka kijiji hadi mmbuga yenyewe.*

Kwa kuwa mazingira ya hifadhi ya Saadani ni Jangwa wafanyabiashara wenye asili ya India chini ya Kampuni ya Albhai Panju and Sons walianzisha kilimo cha zao la chumvi na kuvuna maelfu ya tani waliyoisafisha kwenda maeneo mbalimbali ya nchi.

Kampunu hiyo iliweka kiwanda chake maeneo ya Malumbi nje kidogo ya Bustani ya Wanyama ya Saadan, na baadaye serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa (Stamico) iliweza kuanzisha kiwanda cha kisasa cha uzalishaji chumvi na kupeleka watalaamu wa madini na kuanzisha mradi huo uliokuwa mkubwa sana.

Lakini katika kipindi chote Hifadhi hii iliyopo chini ya TANAPA, iliyoanzishwa mwaka 1962 ikiwa ni pori la akiba na Mwaka 2005, kupandishwa hadhi rasmi na kuwa hifadhi ya taifa, ikashuhudia ongezeko la wahamiaji waliovutwa na upatikanaji wa Samaki aina ya Kamba ambao katika kijiji hicho hujulikana kama Makaji ambayo yalikuwa yakiuzwa kwa bei kubwa na kuwa na maslahi mazuri kwa wavuvi.

Makampuni binafsi kama vile Dar Ocean Product na hata Tafico walikivamia kijiji hicho kwa ajili ya kununua samaki hao kutoka kwa wavuvi wenyewe moja kwa moja.

Lakini katika kipaindi chote hivyo huku zikipita awamu zote tano la utawala wa Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania wana kijiji walikuwa na changamoto mbalimbali za maendelo kama vile ukosefu wa nishati ya umeme na maji.

Kadhalika miundombinu ya barabara inayotokea mwishoni mwa daraja la kisasa la Wami kuingia kulia katika Vijiji vya Mandela na baadaye Miono, Zimbili, Mkange na kuingia Saadan ilikiuwa ipo katika hali mbaya.

Serikali ikaifanyia kazi changamoto hiyo baada ya kufanya ujenzi wa kisasa wa baraba inayotokea eneo la Makurunge Bagamoyo yalipokuwa mashamba ya mifugo ya Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo (RAZABA) hadi kuingia Kijiji cha Saadani kupitia miji iliyokuwa kandoni mwa bahari ya Hindi kama vile Mkwaja na Buyuni.

Katika utawala huu wa awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, Mbunga ya Saadani inang'aa,baada ya kupatiwa umeme wa kutosha.

Kwa takriban mwaka sasa wakazi wa Saadani wanafaidika na uwepo wa nishati ya umeme, waliyoikosa tangu nchi kupata uhuru.

Kufuatia kupatikana kwa nishati hiyo kijiji cha Saadan kilichokuwa kikikumbana na matukio ya kuvamiwa na wanyama wakati na waharibifu kama vile Tembo na Simba sasa imepungua na kuwa sehemu salama toka kijiji hadi mmbuga yenyewe.


Hivi sasa mkazi wa Saadani atakayetafuta bughudha ya kukutana na wanyama ni yule atayekwenda misituni kwa ajili ya kufanya shuguli za kibinadamu kama vile kuzoa chumvi au kuvua katika maeno yasiyokuwa rasmi kwa shuguli hiyo.

Wakazi wa Saadani kwa sasa wanaliimba jina la Rais Samia kwamba ndiye aliyendika historia ya kuing'arisha Saadani, kizazi kipya kutoka eneo hili sasa hakina tena histoiria ya enzi hizo ambazo wakazi walifuata taa aina ya Karabai iliyokuwa ikiwashwa na wafanyabiashara maarufu enzi hizo Mohamed Mwarabu al maarufu Mzee Ganda na Mfaume Akida Mimi na Sheikh Said waliokuwa wakimiliki maduka zama hizo.



# TRUMP AENDELEA KUINYIMA USINGIZI URUSI

NA MWANDISHI WETU



KUREJEA madarakani kwa Donald Trump, ambaye hapo awali aliahidi kumaliza vita nchini Ukraine, kumeibua hali mpya ya wasiwasi miongoni mwa makampuni ya Magharibi ambayo bado yanaendelea kufanya shughuli zake nchini Urusi.

Hali hii inatokea wakati serikali ya Urusi ikiendelea kuimarisha sheria na masharti yanayoongeza gharama za kujiondoa kwenye soko lake, pamoja na kutoa vivutio finyu kwa wanaotaka kuendelea kufanya biashara nchini humo.

Tangu Moscow ilipoivamia Ukraine mnamo Februari 2022, makampuni makubwa kama Renault, McDonald's na Heineken yaliondoka Urusi, yakiuza hisa na mali zao kwa hasara kubwa kufuatia sheria kali zilizowekwa.

Baadhi ya makampuni mengine, hususan yale ya vyakula na bidhaa za usafi kama PepsiCo, Procter & Gamble na Mondelez, bado yanaendelea kufanya shughuli zake nchini Urusi kwa kile wanachokiita "sababu za kibinadamu."

Benki kadhaa za Ulaya kama Raiffeisen Bank International na UniCredit nazo zinajikuta katika mtanziko huohuo, zikikabiliwa na ugumu wa kurejesha mali zao zilizozuiliwa nchini Urusi.

Tayari, serikali ya Moscow inadai punguzo la angalau asilimia 60 wakati wa miamala ya kuondoka, sambamba na 'mchango wa hiari' wa asilimia 35 kwenye bajeti yake, ambao Marekani imeuita "kodi ya kuondoka."

Je, Trump atafanya nini?

Wadau mbalimbali wa kibiashara na kisheria, akiwemo Ian Massey, mtaalam wa biashara, wanasema ushindi wa Trump unaongeza sintofahamu kwa mashirika yenye mali au vitegauchumi nchini Urusi.

Kremlin inatarajiwa kuendelea kuongeza gharama za kujiondoa ili kufidia hasara, huku Trump akitabiriwa kupunguza gharama za uendeshaji kwa makampuni yanayopendelea kuwekeza au kurejea Marekani.

"Inatarajiwa itachukua miezi kadhaa kuumaliza mzozo wa Urusi na Ukraine, hata kama Trump atraingilia kati," anasema Massey. "Hivyo, makampuni yatakuwa yakitathmini mikakati yao kwa umakini zaidi."

Baadhi ya wachambuzi wanaamini kurejea kwa Trump kunaweza kuwapa uwezekano mpya makampuni yanayotaka kuendelea na biashara zao Urusi, ikiwa vikwazo vya kimataifa vitaregezwa. Kwa upande mwingine, huenda yakatokea mazingira yatakayoharakisha makampuni mengine kukamilisha mpango wao wa kujiondoa kabisa.

Sheria za Moscow zinavyozidi kuwa kali

Kwa mujibu wa Alexei Yakovlev, mkurugenzi katika Wizara ya Fedha ya Urusi, mazungumzo ya mikataba ya kuondoka kwa makampuni fulani bado yanaendelea.

Hata hivyo, hakufafanua ikiwa kurejea kwa Trump kunaweza kuzuia hatua za makampuni hayo au kusaidia mengine kurejea nchini Urusi.

Serikali ya Urusi imesisitiza kuwa mpango wowote wa kujiondoa unaohusisha dola milioni 488 au zaidi, lazima upitishwe na Rais Vladimir Putin.

Aidha, wanunuzi wa ndani wanaotaka kununua mali za makampuni ya nje, wanapaswa kuonyesha mkakati mahsusi, likiwemo jinsi gani kununua au kutonunua biashara husika kunavyoweza kuathiri uchumi wa Urusi.

Mustakabali uliojaa sintofahamu

Mengi yamebadilika tangu mwaka 2022, wakati makampuni mengi yalianzisha mazungumzo ya kujiondoa. Kwa sasa, mchakato huo ni mgumu zaidi kutokana na:

Tathmini ya Thamani: Thamani ya makampuni inahitajika kuthibitishwa na wataalam huru wanaoteuliwa na Wizara ya Uchumi ya Urusi.

Minada ya Uwazi: Serikali inaendesha minada ili kuwapa wanunuzi wote wa ndani fursa sawa, jambo linalowapa makampuni ya Magharibi hofu ya kushindwa kupata bei nzuri.

Kurejea kwa Trump madarakani kumebadili kabisa ramani ya kisiasa na kiuchumi, na huenda kukabadilisha mwelekeo wa makampuni ya Magharibi yanayoyumba kati ya kuondoka au kuendelea kubaki Urusi.

Hata hivyo, mwelekeo huu unatabiriwa kuambatana na mifumo mipya ya kisheria inayodhibiti mtiririko wa rasilimali na fedha.

Bado hakuna uhakika juu ya lini vita vya Ukraine vitakoma, au jinsi Trump atakavyoshughulikia mgogoro huo na vikwazo dhidi ya Urusi.

Wakati uamuzi wa mwisho ukisubiriwa, makampuni ya Magharibi yanajikuta kwenye maamuzi magumu zaidi kuliko wakati wowote ule.

Je, yatadumu Urusi, kuondoka sasa, au kusubiri kuona iwapo sera za Trump zitapunguza gharama zao za uendeshaji na athari za vikwazo?

Ni wazi kuwa mustakabali wa uchumi wa kimataifa unazidi kugubikwa na hali ya kutokuwa na uhakika, huku macho ya wachumi na wafanyabiashara wengi yakielekezwa kwenye Ikulu ya Marekani na Kremlin.




# Michezo Kimataifa

## Tetesi za soka




MANCHESTER United wameomba kufahamishwa kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, huku winga wa Argentina Alejandro Garnacho, 20, akihusishwa na uhamisho wa kwingineko.



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.





1

MANCHESTER United huenda ikamsajili mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, kwa mkopo ikiwa Muingereza Marcus Rashford, 27, ataondoka katika klabu hiyo. (The Athletic – Usajili unahitajika)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani





## Masumbwi ya Mama kurindima Dar

NA MWANDISHI WETU

WANAMASUMBWI wa kike wa ngumi za kulipwa pamoja na wengine mbalimbali watashiriki katika mapambano ya mchezo huo utakaofanyika hivi karibuni kulingana na habari zilizolifikia gazeti hili.

Hayo yatakuwa ni maadhimisho mapya ya ngumi ya Wanawake yatakayojulikana kama Samia "SAMIA WOMEN BOXING CHAMPIONSHIP 2025" ambayo yanatarajiwa kauanza Ijumaa 31-01-2025 mpaka 02-02-2025 katika fukwe za Kawe Beach Club, Dar es salaam.

Mashindano hayo yaliyoasisiwa na Shirikisho la Ngumi Tanzania (BFT) yanalenga kuongeza hamasa kwa Wanawake katika mchezo wa ngumi nchini, pia yatatumika kuchagua wachezaji watakao jiunga na kikosi cha Timu ya Taifa itakayojiandaa kushiriki kwa mara ya pili k Mashindano ya 14 ya Ubingwa wa Dunia yatakayofanyika Nichini Serbia kuanzia Tarehe 06-03-2025 mpaka 17-03-2025.

"Hii itakua ni mara ya pili kwa Taifa kushiriki mashindano ya Ubingwa wa Dunia, baada ya kufanya hivyo kwa mara ya kwanza kwanye mashindano ya 13 yalifanyika New Delhi, India mwezi wa tatu, 2023... Maandalizi ya mashindano yetu yanaendelea vizuri, tunawaomba wadau mjitokeze kwa wingi kutuunga mkono kwa hali na mali" Alinukuliwa Asha George Voniatis, Mwenyekiti wa kamati ya wanawake na wachezaji ya BFT na mjumbe wa kamati ya usawa kijinsia ya Afrika (AFBC).

Mashindano haya yatashirikisha wachezaji wanawake wanaocheza ngumi za ridhaa na za kulipwa kupitia kamisheni ya ngumi za kulipwa (TPBRC)

Pamoja na mashindano hayo, wachezaji wote watahudhuria semina za kuwawezesha, kuwajengea maarifa ya maisha na Ujasiliamali kwa kushirikina na taasisi ya ARHN ya Mbezi Beach, Dar es salaam.

# Burudani



## Msondo Ngoma wamwimbia Dkt Samia

NA MWANDISHI WETU

BENDI kongwe ya muziki wa dansi Msondo Ngoma wiki hii imemaliza mazoezi ya wimbo maalum waliouandaa kwa ajili ya kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, wimbo huo ambao umeanza kupingwa katika maeneo mbalimbali inapofanya maonyesho yake ya wiki, umeanza kuwa kivutio kwa mashabiki.

Akizungumza na gazeti hili Meneja wa bendi hiyo Saidi Kibiriti alisema, hao kama Tasisi wameona juhudi za makusudi zinazofanywa na kiongozi huyo na kuona ipo sababu ya kumpa maua yake.

Naye mkuu wa Jukwaa wa bendi hiyo Juma Katundu alisema kuwa katika wimbo huo wanazungumzia baadhi ya manufaa waliyopata Watanzania katika kipindi cha Utawala wa awamu ya sita kama vile ujenzi wa reli ya kisasa pamoja na usafiri wa Treni ya umeme, pia miundombinu na ukuaji wa uchumi mambo ambayo kwa sasa yanaonekana hata kwa macho.

Alisema wimbo huo utakapokamilika watairekodi na kisha kuusambaza katika vituo vya redio na Televisheni ili Watanzania waone kazi hiyo iliyolenga kutoa wasifu na kuzitambua juhudi zinazofamnywa na viongozi katika mikakati ya kuendeleza taifa la Tanzania.

Alisema huo ni mwanzo lakini bendi hiyo itakuwa ikitunga nyimbo kama hizo kwa ajili nya viongozi mbalimbali na hata watu wengine wanaojitolea kusaidia masuala ya kijamii katika nchi hii.



## Belle 9 ammwagia sifa Ben Pol

NA EMMANUEL TAIRO

STAA wa RnB Bongo, Abednego Damian 'Belle 9', ameweka wazi kuwa, katika utaratibu wake wa kufanya kazi haangalii wala kuchagua wa kufanya naye.

Belle 9 ambaye aliwahi kutamba na ngoma ya 'Sumu ya Mapenzi "Najua watu huwa tunasahau fadhila na mimi kiukweli nisiwe mchoyo wa kutoa shukurani, ninamshukuru sana, Ben Pol kwa mambo aliyoweza kunifanyia mpaka hapa nilipofikia.

"Alikuwa mwalimu mzuri sana kwangu na alikuwa anapenda nitimize ndoto zangu, hakutaka nikate tamaa kabisa," anasema Belle 9

Mwimbaji huyo ameliambia Gazeti la Jamvi la Habari kuwa, msanii anayejiamini kwenye kazi zake haoni sababu ya kuanza kuchagua watu wa kufanya nao kazi, bali kuona wasanii wachanga wanafika mbali.

## Mlela: Sanaa inatakiwa ikue

NA EMMANUEL TAIRO

MKALI katika tasnia za filamu, Yusuf Mlela amesema kutokana na mabadiliko yanayohitajika kwenye sanaa, haoni tatizo wasanii wa Bongo Fleva wakiingiza kwenye filamu na tamthiliya.

Akizunguza na mwandishi wa gazeti hili, Mlela ambaye ukiachilia mbali na uigizaji pia ni muongozaji wa tamthilia, amesema kuwa sanaa kila siku inatakiwa ikue ndiyo maana wasanii wengi wa Bongo Fleva wameamua kufanya hivyo.

"Unajua sanaa inatakiwa ikue kila siku mambo yanatakiwa mapya, ukiangalia sisi wote ni wasanii na msanii lazima aweze kuonyesha uwezo wake katika sanaa, acha waingie ili kuleta vitu vya tofauti," alisema Mlela.

## Jb atamani waigizaji wapya

NA ERYNE BANDA

MSANII mkongwe wa Bongo Movie, Jacob Steven 'JB', amesema sababu za maprojuza kurudia wasanii wale wale kwenye filamu na tamthilia ni kutokana na uwepo wa waigizaji wachache wenye uwezo huo.

JB alisema atamani wapate waigizaji wapya wenye uwezo mkubwa zaidi, ndiyo maana yuko bize kufanya usaili wa waigizi wapya ili kuleta sura mpya kwenye uigizaji kwani mashabiki wamechoka kuona waigizaji ni wale wale hawabadiliki.

"Mashabiki wasitulaumu sana kwa maprojuza kurudia wasanii wale wale kwenye filamu na tamthilia. Sababu ni tasnia ya uigizaji ina waigizaji wachache wenye uwezo wa kuigiza. Ndiyo sababu mashabiki wanaona hawabadiliki.

Binafsi nimeligundua hilo na natamani nipate waigizaji wapya wenye uwezo mkubwa zaidi, ndiyo maana niko bize sasa hivi kufanya usaili wa waigizi wapya ili kuleta sura mpya kwenye uigizaji," alisema JB.



JAMVI LA HABARI
SPOTI
JUMATANO JANUARI 29, 2025



**Khadija Kopa awasha moto ndoa ya Zuchu na Diamond**

>> Soma Uk. 15

# AZIZ KI NI YANGA DAMU



NA MWANDISHI WETU

KLABU ya Yanga imewataka mashabiki wake wapuuze taarifa zinazosambazwa na wabaya wao katika mitandao ya kijamii, zikidai kiungo wao mshambuliaji Aziz Ki, anatarajia kuaiacha timu hiyo na kwenda kutafuta changamoto nyingine.

Taarifa hizo zimekuwa zikirudia kusambazwa katika mitandao tofauti, imeleta taharuki kwa mashabiki wa timu hiyo, kwa vile mchezaji huyo ni moja kati ya nyota wanaotumainiwa katika kikosi cha timu hiyo.

Katika taarifa hiyo inadaiwa kuwa, Aziz Ki hakupendezewa na timu yake Yanga, kutolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa hatua ya 16 Bora, hivyo anatamani kuondoka ili akaitumikie klabu itakayocheza michuano mikubwa ya kimataifa.

Taarifa hizo zimekanusha vikali na klabu hiyo, ikisisitiza kuwa ni za kupuuzwa kwa vile zinalenga kuwasambaratisha mashabiki.

Hata hivyo kiongozi mmoja wa Yanga aliyeongea na gazeti hili kwa masharti ya kutotajwa jina lake alisema, wamechelewa kukanusha kupitia mitandao ya Jamii kutokana na kutokuwepo kwa Meneja wake wa Habari na Mawasiliano Ali Kamwe aliyekwenda nchini Morocco kushiriki Droo ya michuano ya Afcon.

## Simba yakomalia uraia kwa wachezaji wake

NA MWANDISHI WETU

KLABU ya Simba imekiri kupiga hodi katika ofisi za Uhamiaji kwa ajili ya kuwaombea Uraia wa Tanzania wachezaji wake tisa wa kigeni, wanaoitumikia timu hiyo katika msimu huu wa Ligi Kuu.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo Ahmed Ali alisema, ni kweli klabu yao imechukua hatua hiyo kutokana na maridhiano baina ya wachezaji hao na uongozi wa Simba.

Kanuni za Shirikisho la Soka Tanzania linaruhusu klabu kusajili wachezaji 12 wa nje, hivyo endapo Simba itafanikiwa kuwapatia uraia wachezaji wake hao itakuwa na upungufu wa wachezaji 9, hivyo itakuwa na uwezo wa kusajili tena idadi hiyo.



Hatua hii imekuja siku chache baada ya klabu nyingine inayocheza Ligi Kuu Singida Big Stars, kuwapatia uraia wachezaji wake watatu wa kigeni wanaoitumikia timu hiyo.

wafuatialiaji wa michezo waliozungumza na gazeti hili wamedai kuwa hatua hiyo ni nzuri kwa vile haitakuwa na faida kwa timu pepekee bali pia itaimarisha kikosi cha timu ya Taifa (Taisa Star) ambayo itashiriki michuano ya Afcon Tanzania ikiwa miongoni mwa waandaaji.




## Waandaaji AFCON 2027 Wapikwa chungu kimoja

WAANDAAJI wa michuano ya Afcon mwaka 2027, timu za Taifa za Tanzania (Taifa Stars) na Uganda (The Crane) zimejikuta zikipangwa katika kundi moja, katika michuano ya mwaka huu 2025 itakayofanyika Morocco.

>> Inaendelea Uk. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM